**HOTUBA YA KATIBU MTENDAJI WA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI WAKATI WA UFUNGUZI WA MAONESHO YA MIFUKO YA UWEZESHAJI YATAKAYOFANYIKA KATIKA VIWANJA VYA MWENGE CENTRE KIGOMA KUANZIA TAREHE 21-27 MEI, 2023**

- ***Mheshimiwa Thobias Andengenye, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma;***
- ***Mhandisi Albert Msovela Gabriel, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma;***
- ***Viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa;***
- ***Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri mliopo;***
- ***Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;***
- ***Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali;***
- ***Wakuu wa Taasisi zinazosimamia Mifuko na Programu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi za Serikali na za sekta binafsi;***
- ***Wawakilishi kutoka katika taasisi mbalimbali za sekta binafsi;***
- ***Waratibu wa Uwezeshaji wa Wananchi katika Uwekezaji;***
- ***Wanahabari;***
- ***Wageni Waalikwa;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***ITIFAKI IMEZINGATIWA***

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*!***

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mgeni Rasmi, kwa kukubali kutufungulia Maonesho haya. Aidha, nawashukuru viongozi na watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma chini ya Uongozi Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa ushirikiano mkubwa katika kuandaa Maonesho haya na pia kwa makaribisho mazuri mkoani Kigoma. Nawashukuru pia wote walioalikwa na kuweza kuja kushuhudia ufunguzi wa Maonesho haya. Tunatambua kuwa nyote mnayo majukumu mengi mliyopanga kuyafanya siku ya leo lakini pamoja na

hayo mmeweza kukubali mwaliko wetu na kuja kushiriki katika ufunguzi wa Maonesho haya. ***Nawakushukuru Sana.***

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Natoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa kamati ya maandalizi ambayo iliyojumuisha wataalamu kutoka mifuko na programu mbalimbali za uwezeshaji na wataalamu kutoka Mkoa wa Kigoma kwa kazi nzuri waliyofanya bila kuchoka na kuhakikisha Maonesho haya yanafanyika kama yalivyopangwa. Kwa kipekee napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadhamini wa Maonesho haya na kipekee natoa shukurani za dhati kwa wakuu wa taasisi zinazosimamia mifuko na program za uwezeshaji za Serikali na sekta binafsi kwa michango yao ya hali na mali katika kukuza uwezeshaji na kufanikisha Maonesho haya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Maonesho ya sita ya mifuko na programu za uwezeshaji katika Kanda ya Magharibi imehusisha Mkoa wa Katavi lakini pia Mikoa mingine ya jirani imeshiriki pia. Maonesho ya kwanza yalifanyika mwaka 2017 katika Kanda ya Kati iliyohusisha Mkoa wa Dodoma, Singida na Tabora; Maonesho ya pili yalifanyika mwaka 2018 katika Kanda ya Nyanda za Juu iliyohusisha Mkoa wa Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Ruvuma na Songwe; Maonesho ya tatu yalifanyika Mwaka 2019 katika Kanda ya Ziwa na yalihusisha Mkoa wa Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu na Shinyanga; Maonesho ya nne yalifanyika mwaka 2021 katika Kanda ya Kaskazini iliyohusisha Mkoa wa Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga; na Maonesho ya Tano yalifanyika mwaka 2022 katika kanda ya Mashariki iliyohusisha Mkoa wa Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa miaka mingi Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa lengo la kujenga uchumi na kuwaondoa wananchi katika umaskini. Juhudi hizo ni pamoja na kuanzisha mifuko na program za uwezeshaji mbalimbali kwa lengo la kutoa mikopo au dhamana ya mikopo kwa wananchi kwa masharti nafuu, kutoa ruzuku pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi ili waweze kukopesheka au kuhudumiwa na wadau wengine.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Hadi Machi, 2023, Mifuko na Programu za Uwezeshaji zinazoratibiwa na Baraza zimefikia 72 zikihusisha mifuko ya Mikopo ya moja kwa moja, Mifuko ya dhamana, mifyuko ya ruzuku na Programu za Uwezeshaji ambayo imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Trioni 6.1 kwa wajasiriamali **8,650,257** wakiwemo wanawake **4,747,321** na wanaume **3,902,936**. Aidha, mifuko na programu hizi zimetengeneza jumla ya ajira **17,603,271** ambapo ajira kwa wanawake zilikuwa **9,248,916** (52.5%) na ajira kwa wanaume ni **8,354,355** (47.5%).

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Maonesho ya mwaka 2022 yana Kaulimbiu isemayo:***" UWEZESHAJI KIUCHUMI KUPITIA MABADILIKO YA KIDIGITALI"*** ambayo inaakisi hali ya mabadiliko ya kidigitali kwa sasa ambapo mabadiliko hayo yatawezesha kufikisha fursa za uwezeshaji kwa haraka na kuenea maeneo mengi zaidi kupitia mifumo ya kidigitali na taasisi zinazosimamia mifuko na programu za uwezeshaji za Serikali na za sekta binafsi zimeshaanza kutumia mifumo hii kutangaza vigezo, sifa, masharti, taratibu za kunufaika na mikopo hii; na walengwa wa mifuko na programu za uwezeshaji wameanza kufikiwa kwa urahisi zaidi na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa mifuko hii.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Miongoni mwa matokeo yanayotarajiwa kutokana na Maonesho haya ni: kukuza uelewa wa wananchi walio wengi kuhusu kuwepo kwa mifuko na programu za uwezeshaji; kuongezeka kwa utamaduni wa kujiwekea akiba na kuwekeza katika miradi ya kiuchumi yenye kuleta faida; na kuongeza hamasa kwa wananchi kutafuta vigezo vya kukopesheka ikiwa ni pamoja na kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi kama SACCOS na VICOBA.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba nichukue nafasi hii tena kuipongeza Ofisi ya Mkoa wa Kigoma, wananchi wa Mkoa wa Kigoma na wadhamini wa Maonesho kwa kufanikisha Maonesho ya Sita ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji mwaka 2023. Sisi kama waratibu wa mifuko na programu za uwezeshaji tunakuhaidi kuwa tutaendeleza ushirikiano ili kuongeza shughuli za kiuchumi kwa lengo la kupunguza mzunguko wa umaskini katika jamii.

***Mheshimiwa* Mgeni Rasmi*, baada ya kusema hayo, ninaomba kuwasilisha***

***Nawashukuru Sana kwa Kunisikiliza***